TANGAZO LA SERIKALI NA 332 la Tarehe 20/07/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

———

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

———

SHERIA NDOGO ZA (ADA ZA VIBALI VYA BURUDANI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika	1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.
Tafsiri	3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo
	"Ada" maana yake ni kiasi cha fedha kitakachotozwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya kibali cha shughuli ya burudani,itakayofanyika katika eneo la Halmashauri;
	"Afisa mwidhinishaji" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; **"Eneo la Burudani**" ni mahali popote ambapo shughuli ya burudani inafanyika. **"Halmashauri"** maana yake ni Halmashauri ya

	Manispaa ya Kigamboni **"Kibali cha burudani"** Maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za burudani katika ukumbi, uwanja wa michezo au sehemu yoyote ya wazi au Mitaani. **"Mkurugenzi"** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi. **"Muda wa burudani"** Maana yake ni wakati ambao umetajwa katika kibali wa kufanyika shughuli ya burudani kufanyika. **"Muda wa watoto"** Maana yake ni wakati wa mwisho kwa watoto kuwepo katika eneo la burudani ambao ni saa kumi na mbili jioni. **"Shughuli ya burudani"** maana yake ni sherehe , shughuli yeyote ile ya kijamii, michezo na muziki isipokuwa kusanyiko la misiba "
Wajibu wa kuwa na Kibali	4. Mtu yeyote hatoruhusiwa kuendesha shughuli yeyote ya burudani ndani ya eneo la Halmashauri bila ya kupata kibali kutoka Halmashauri.
Utaratibu wa kuomba kibali	(1) Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli ya Burudani katika eneo la Halmashauri atatuma maombi ya maandishi kwa Mkurugenzi kwa kupitia kwa Mtendaji wa Mtaa husika kwa kujaza fomu iliyoambatishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi. (2) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yataeleza jina la mwombaji, aina ya burudani, tarehe, muda wa kuanza na kumalizika kwa burudani na eneo husika.

	(3) Iwapo maombi ya kibali yatakataliwa Halmashauri itamuarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa kutoa kibali.
Ada ya maombi ya vibali	Maombi yote ya vibali yatalipiwa Ada kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.
Vigezo vya utoaji wa vibali	Halmashauri haitatoa kibali hadi itakapojiridhisha na mambo yafuatayo:- (a) shughuli ya burudani inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani. (b) eneo linaloombewa kibali cha kufanyia shughuli ya buradani linaruhusiwa kwa shughuli inayombewa kibali. (c) kumbi za burudani zina usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo madirisha ya kutosha ya hewa, milango ya dharura, umeme, milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura.
Mamlaka ya Halmashauri	(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia mahala popote panapofanyika shughuli ya burudani au inapoaminika kuna shughuli ya burudani kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafuata masharti ya kibali. (2) Katika kutekeleza Mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1) Afisa wa Halmashauri atakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli ya Burudani kulingana na hali itakayobainika katika ukaguzi.
Mkusanyiko wa watoto	(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukusanya watoto kwa ajili ya shughuli yoyote ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi

	cha Halmashauri. (2) Mkusanyiko wowote wa watoto uliopata kibali cha Halmashauri kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) utamalizika kwa kuzingatia muda wa watoto.. (3) Mtu yeyote aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atawajibika juu ya usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko huo na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko. (4) Itakuwa ni makosa kwa mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye mamlaka juu ya mtoto kuruhusu au kusababisha kwa uzembe mtoto kuhudhuria mkusanyiko usio na kibali cha Halmashauri.
Vibali visivyotozwa Ada	Mikusanyiko ifuatayo itaombewa vibali bila kulipa ada,:- (i) Mikusanyo ya kidini (ii) Misiba (iii) Michezo ya watoto isiyotozwa
Usafi wa mazingira	(1) Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za burudani atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya burudani kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli ya burudani.
Mziki unaoleta kero	Mtu yeyote aliyepata kibali cha burudani hatoruhusiwa kupiga muziki unaoleta kero kwa majirani na jamii kwa ujumla kwenye eneo lake la burudani.
Adhabu	Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi

	miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote kwa pamoja.
Kufifilisha	Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi elfu thelathini (30,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa na kujaza fomu iliyoambatishwa katika Jedwali la tatu Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 5(1))

JEDWALI LA PILI
CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (2)
MAOMBI YA KIBALI CHA BURUDANI

1. Jina la mwombaji
……

2. Anwani/ Namba ya simu ya mwombaji
……

3. Maombi ya
……

4. Aina ya Burudani
……

5. Muda unaoomba kwaajili ya Burudani
……

6. Saini ya Mwombaji
……

7. Tarehe
……

MAONI YA UONGOZI WA MTAA ATAKAPOFANYIA BURUDANI / ONYESHO

……

……

……

……

Tarehe …….. Muhuri ……

Jina la kiongozi wa Mtaa ……Sahihi……..…

JEDWALI LA PILI

(Limetungwa chini ya kifungu cha 6)

NA	AINA YA BURUDANI	ADA KWA KILA

		ONESHO/TUKIO TSHS
1	ONESHO LA MUZIKI	100,000/= kwa siku
2	ONESHO LA MICHEZO YA KUIGIZA	50,000/=kwa siku
3	MUZIKI WA DISKO	50,000/=kwa siku
4	MUZIKI WA TAARABU	50,000/=kwa siku
5	SHEREHE ZA MASHIRIKA NA TAASISI MBALIMBALI	50,000/=kwa siku
6	ONESHO LA CINEMA	50,000/=kwa siku
7	**SHEREHE MBALIMBALI (Kwa siku)**	20,000/=kwa siku
8	KUREKODI MKANDA TV	50,000/=kwa mkanda
9	VIDEO	30,000/=kwa mwezi
10	TAMASHA LA NGOMA ZA ASILI	20,000/=kwa siku
11	MATUMIZI YA ENEO LA WAZI	50,000/=kwa siku
12	DANCE	100,000/= kwa siku
13	MAONESHO YA SANAA/COMEDY	100,000/= kwa siku
14	POOL	50,000/= kwa mwaka
15	USHURU WA TIBA ASILIA	50,000/= kwa mwaka
16	BAHATI NASIBU	30,000/= kwa mwezi
17	KOROKORO/TOMBOLA/FETE	30,000/= kwa mwezi
18	MATUMIZI YA UWANJA WA MPIRA	500,000/=/30% ya mapato
19	**BETTING**	200,000/= kwa mwezi
20	BAHATI NASIBU YA SANDUKU	100,000/= kwa mwezi
21	STUDIO YA KUREKODI SANAA	50,000/= kwa mwezi

22	SANAA ZA UFUNDI	20,000/= kwa mwezi
23	MASHINDANO YA UREMBO	100,000/= kwa tukio
24	MATANGAZO MITAANI KWA KUTUMIA SPIKA	50,000/= kwa siku

JEDWALI LA TATU

KUFIFILISHA KOSA

Limetungwa Chini ya kifungu cha 14

Mimi……..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya……ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwamba mnamo tarehe……ya mwezi……..mwaka ……nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Ada ya Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……ya mwezi……Mwaka……..

Jina……..

Saini…….

Mbele ya:

Jina……..

Cheo……

Saini……

……

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigamboni imebandikwa kwenye Sheria Ndog
hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnam
tarehe .31 Januari, 2018 mbele ya:-

.....

STEPHEN E. KATEMB

MKURUGENZ
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBON

MUHURI

.....
MAABAD SULEIMAN HOJ
MSTAHIKI MEY
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBON

NAKUBALI

.....
MHE. SELEMANI S. JAFO {M
WAZIRI WA NCHI/OR TAMISE/

DODOMA
TAREHE ....., 2018